**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII**
**JINSIA, WAZEE NA WATOTO**

# TAARIFA KWA UMMA

## TAARIFA YA WAGONJWA WAPYA WALIOTHIBITIKA KUWA NA MAAMBUKIZI YA VIRUSI VYA CORONA (COVID-19) NCHINI

Ndugu Wananachi,

Ninapenda kutoa taarifa ya mwenendo wa maambukizi ya virusi vya Corona (COVID-19) nchini katika kipindi cha masaa 24 yaliyopita baada ya taarifa yangu ya jana.

Wagonjwa wapya **02 (wawili)** wamethibitka jijini Dar es Salaam kuwa na COVID-19, na hivyo kufanya jumla ya wagonjwa waliothibitika nchini mpaka sasa kufikia **06 (sita),** ambapo mmoja ni yule wa Zanzibar aliyetolewa taarifa jana.

Mchanganuo wa wagonjwa hao wapya wawili ni kama ifuatavyo:

- Mwanaume, Mtanzania, mwenye umri wa miaka 40 aliyesafiri nchi za Uswisi, Denmark na Ufaransa kati ya tarehe 05 Machi 2020 hadi tarehe 13 Machi 2020 na kurudi nchini tarehe 14 Machi 2020;
- Mwanaume, Mtanzania, mwenye umri wa miaka 40, ambaye alisafiri Afrika ya Kusini kati ya tarehe 14 machi 2020 hadi tarehe 16 Machi 2020 na kurejea nchini usiku wa tarehe 17 Machi 2020.

Wahusika wote wametengwa (isolation) na hali zao zinaendelea vizuri. Juhudi za kufuatilia watu waliokuwa karibu na wagonjwa waliothibitika kuwa na COVID-19 (yaani “contacts”) zinaendelea. Hadi sasa jumla ya watu 46 wanafuatiliwa jijini Arusha, na watu 66 wanafuatiliwa jijini Dar es Salaam

Asanteni sana.

**Ummy A. Mwalimu (Mb)**
**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII,**
**JINSIA, WAZEE NA WATOTO**
**19 Machi 2020**